**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUANZISHA MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naanza kuwasilisha Hotuba yangu hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uhai na afya njema, ambayo imetuwezesha kukamilisha jukumu muhimu la Nchi yetu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu Azidi kutubariki amani na upendo, busara na hekima, pamoja na neema zake zote ambazo kwa hakika sisi ni wahitaji kutoka kwake.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia, kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati yetu katika Baraza hili tukufu kwa ajili ya kuuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee natanguliza shukurani za Kamati kwake Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa mashirikiano na nasaha zake tangu hatua za awali za mafunzo hadi tunakamilisha kazi hii muhimu na adhimu mbele ya Baraza Lako.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa, natoa shukurani zetu maalum kwa uongozi mzima wa Wizara ya Afya pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mashirikiano yao makubwa wanayoipatia Kamati na kupelekea kazi ya kuupitia na kuujadili Mswada huu kuwa nyepesi kwetu.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mashirikiano yao makubwa waliyotoa kwangu na juhudi zao wakati wa kuujadili kwa kina Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa kwa ruhusa yako niwatambulishe Wajumbe wa Kamati hii kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Mohammed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | Makamo Mwenyekiti |

| | | |
|---|---|---|
| *3.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zawadi Amour Nassor | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mussa Issa Musa | Katibu |
| *9.* | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,** Natumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wadau wote waliofika mbele ya Kamati kuja kutoa maoni yao pamoja na michango mbali mbali yanayohusiana na Mswada huu kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 84(7) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020 kwa lengo la kuuimarisha ili baada ya kupitishwa iwe Sheria nzuri na yenye kutekelezeka kwa walengwa wote.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa Wadau walioshiriki kutoa maoni ya ni:

1. Mjumbe kutoka Washirika wa Maendeleo;
2. Mjumbe kutoka Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar (ZATUC);
3. Mjumbe kutoka Jumuiya ya Wastaafu na Wazee Zanzibar (JUWAWAZA);
4. Mjumbe kutoka Jumuiya ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Zanzibar (ZAHILFE); na

5. Mjumbe kutoka Baraza la Wauguzi na Wakunga Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo ambayo yamejikita zaidi katika kuweka sawa lugha iliyotumika, kutoa tafsiri kwa baadhi ya maneno inayolingana na uhalisi, kuanzisha kifungu kipya kinachotoa uwezo wa Bodi kuanzisha Hesabu (account) yake pamoja na kuweka sawa adhabu zilizoainishwa ili ziweze kuendana na uzito wa kosa husika.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, naomba kuwaeleza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi na msisitizo wa baadhi ya vifungu ambavyo vimependekezwa kufanyiwa marekebisho na Kamati kutokana na ubora wa mswada wenyewe. Hivyo, maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika marekebisho ya Kamati ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa ili kujisomea kwa ufafanuzi na ufahamu zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha *3* cha Mswada huu Kamati inashauri kufutwa tafsiri ya neno *"Mnufaika"* ili kuondoa utata wa matumizi ya neno hilo hapo baadae kwa sababu neno hili katika Mswada mzima halijatumika katika sehemu wala kifungu chochote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inapendekeza tafsiri ya neno "*Mtegemezi",* kurekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuendana na dhana nzima ya utegemezi kwa wanachama wa Mfuko. Marekebisho hayo yamependekezwa ili kuweka wazi mtegemezi gani atakayehusika baada ya mwanachama kujiunga na Huduma za Mfuko huu wa Afya kwani tafsiri ya awali ilikuwa inajumuisha watu wachache tu na kutojumisha watu wa karibu wa mwanachama kama Mume au Mke wa mwanachama husika. Kamati inapendekeza tafsiri hiyo isomeke kama ifuatavyo:

**"Mtegemezi" maana yake:**

**(a) Mtoto wa kuzaa mwenyewe;**

**(b) Mtoto wa kuasili au kulea ambae mahitaji yake ya lazima yapo chini ya usimamizi wa mwanachama;**

**(c) Mwenza au Mzazi ambae hayupo katika sekta rasmi au isiyo rasmi na hana kipato cha kuchangia."**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inatambua kwamba moja kati ya majukumu ya Katibu wa Bodi ni kuandaa agenda za vikao vya Bodi husika. Kwa kufahamu umuhimu huo, Kamati ya Ustawi wa Jamii inapendekeza kifungu cha 10(3)(a) kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka "kuandaa agenda pamoja na kuchukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi".

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kifungu cha *20* kifanyiwe marekebisho katika kifungu kidogo cha *(2)* kwa kufutwa neno *"thelathini"* na kuwekwa badala yake neno *"Tisini".* Kamati inapendekeza marekebisho hayo ili kutoa fursa kwa Serikali kupata muda muafaka wa kufanya maandalizi ya utekelezwaji wa Sheria hii. Kubakia kama ilivyo awali ingeleta ugumu katika utekelezaji wa Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Kamati pia inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kidogo kipya cha 35(1) kinachoelezea kuanzishwa kwa hesabu ya benki ya Mfuko wa Huduma za Afya. Hili limependekezwa ili fedha zitakazokusanya ziweze kuwa na sehemu maalum ya kuhifadhiwa. Kutokuzingatia hili, Mfuko utakuwa unafanya makusanyo ya fedha zake lakini hakuna eneo ambalo limeainishwa wazi wapi makusanyo hayo yahifadhiwe. Kamati inashauri kifungu kidogo hicho kisomeke "**Mfuko, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, utafungua hesabu ya benki na kuweka fedha zake kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi ulizopewa chini ya Sheria hii."**

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Kamati kimebaini kuwepo kwa adhabu zinazolingana katika kifungu cha 41 kinachoelezea Makosa na Adhabu na kifungu cha 43 kinachoelezea Adhabu ya Jumla. Ili kuondosha mlingano huo, Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kifungu cha 41 kwa kufuta adhabu

iliyopo na kuwekwa faini isiyopungua Milioni Mbili au kifungo kisichopungua Mwaka Mmoja.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Afya baada ya Mswada huu kupitishwa na Baraza lako Tukufu kuharakisha utungaji wa Kanuni mbali mbali zilizotajwa katika vifungu vya Mswada huu ikiwemo kifungu cha 22, 26, 27, 28, 32 na 51 kwani kama inavyofahamika kuchelewa kuwepo kwa Kanuni hizo kutapelekea kushindwa kutekelezeka kwa Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa na kwa upekee mkubwa Kamati yangu inachukua fursa hii adhimu kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuja na Mswada huu muhimu kwa maslahi ya kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya na endelevu kwa wananchi wote wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Ni imani yangu kuwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu watakubaliana na maoni yote ya yaliyotolewa na Kamati kupitia Mswada huu, kwa kubaini maeneo mbali mbali ya kuishauri Serikali kuhusu utekelezaji bora wa Sheria inayotarajiwa kutungwa amabayo itatoa fursa kwa taasisi zinazohusika na sheria hizi kutekeleza majukumu yake

ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati yetu inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwamba Mswada huu uliombele yetu waujadili na kuuchangia ipasavyo na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itaziwezesha taasisi hizi kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii, Naomba kuwasilisha.

Ahsante,



..............................................

(***Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis***)
Kny: Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
Baraza la Wawakilishi,
**<u>Zanzibar.</u>**